

BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz



SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

TAARIFA YA SHUGHULI ZA MKUTANO WA KUMI NA TATU WA BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI UTAKAOANZA TAREHE 6 FEBRUARI, 2019

Mkutano wa Kumi na Tatu wa Baraza la Tisa la Wawakilishi Zanzibar unatarajiwa kuanza siku ya Jumatano tarehe 6 Februari, 2019, saa 3:00 asubuhi.

SHUGHULI ZITAKAZOFANYIKA.

Shughuli za Mkutano huo zitakuwa kama ifuatavyo:-

1. Maswali na Majibu.

Maswali 146 yameratibiwa kwa ajili ya kujibiwa kwenye Mkutano huu.

2. Miswada ya Sheria

Miswada ya Sheria iliyowasilishwa na kusomwa kwa mara ya Kwanza katika Mkutano wa Novemba, 2018 itasomwa kwa mara ya pili na kujadiliwa katika Mkutano huu wa Kumi na Tatu.

Miswada yenyewe ni:-

- i) Mswada wa Sheria ya Marekebesho ya Sheria Mbalimbali ya mwaka 2018 na mambo mengine yanayohusiana na hayo.
- ii) Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Serikali wa huduma za Matrika na Zana za Kilimo, 2018 na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

3. Uwasilishwaji wa Ripoti za Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa Mwaka 2018/2019.

4. Mwelekeo wa Mpango wa Taifa.

5. Ripoti ya Kamati Teule ya Kuchunguza majengo ya Skuli 19 za Sekondari.
6. Taarifa ya Serikali kuhusu Hoja ya Mjumbe kuliomba Baraza la Wawakilishi kutoa maazimio ya kushughulikiwa kwa haraka tatizo la kuharibika kwa vifaa tiba vya Hospitali ya Abdulla Mzee ya Mkoani Pemba.

Raya Issa Msellem
KATIBU
BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR

4 Februari, 2018